

NDOA ZA UTOTONI

TANZANIA

NDOA ZA UTOTONI

ni muungano wa jadi, dini au isiyo rasmi ambapo ama bibi au bwana harusi ni chini ya umri wa miaka 18, mara nyingi ni msichana mdogo akiwa na mwanaume mzee.

“Sijasoma shuleni kwasababu baba yangu aliona hakuna maana ya kumsomesha msichana, kwahiyo baada ya kufanyiwa ukeketaji niliolewa. Baba yangu alipokea mahari na hii ilinilazimisha kuolewa nikiwa na miaka 12. Mama yangu alikubali kwamba nilikuwa mdogo sana, lakini hakuweza kwenda kinyume na maamuzi ya baba yangu akiwa anaogopa kupigwa...”

“...niliolewa nikiwa na miaka 12. Hii ilikuwa kwa ridhaa yangu kwasababu hali ya nyumbani ilikuwa ngumu sana.”

“Ni wazazi ambao wanaamua wasichana wao waolewe, hii ni kwasababu wanajikuta na changamoto nyingi kama umaskini unaowafanya washindwe kuridhisha mahitaji ya kimsingi ya familia zao... Mara nyingine wasichana wenyewe wanaamua waolewe kutokana na hali mbaya ya maisha yao na wanaamini kwamba kuolewa itawaokoa maishani.”

UTAFITI

Utafiti huu ulifanyiwa katika mikoa 10 Tanzania:
SHINYANGA, TABORA, MARA, DODOMA, LINDI, MTWARA, MANYARA, COAST REGION, DAR ES SALAAM NA IRINGA

Mikoa ilichaguliwa kwa idadi ya ndoa za utotoni ambazo zimetokea kutokana na utafiti uliyofanyika zamani; Mikoa 5 ikiwa na idadi kubwa ya ndoa za utotoni, mikoa 3 ikiwa na kiwango cha wastani cha ndoa za utotoni na mikoa 2 ikiwa na idadi ndogo ya ndoa za utotoni. Mikoa hii ilichaguliwa katika utafiti huu ili kulinganisha majibu ya utafiti.

3,299
washiriki

199
mahojiano

190
washiriki katika majadiliano ya vikundi

TATIZO

1. Ndoa za utotoni mara nyingi hutokea kati ya msichana mdogo na mwanaume mzee. Msichana anakuja kunyimwa haki yake ya kuchagua mwenzi na kupewa uwezo mdogo nyumbani na hata **KUNYANYASWA**.

2. Ndoa za utotoni husababisha wasichana **WAACHE SHULE** na, wakiwa hawana elimu, wasichana wanakuwa na fursa chache za kupata kipato.

3. Mtoto aliyepewa malezi na mama ambaye ni mdogo na asiyesoma mara nyingi huingia katika umaskini. Hii ndiyo maana ndoa za utotoni **HUENDELEZA UMASKINI**.

4. **UKOSEFU WA ELIMU** na kutokuwa na uwezo wa kusoma husababisha wasichana wasiwe na namna ya kupata wala kuelewa maelezo kuhusu afya ya uzazi na uzazi wa mpango.

5. Wasichana wakianza kuzaa mapema wanakuwa na muda mchache wa **KUJIFUNZA NA KUJIENDELEZA**. Hii inasababisha wao kuwa na uwezo mdogo wa kulea watoto wao au kuchangia katika jamii yao.

6. Wasichana wanaoingia katika ndoa mapema uwa wanaingia katika ujauzito mapema. Hii inawaweka katika hali ya **HATARI ZAIDI WAKATI WA UJAUZITO NA KUJIFUNGUA**. Kwa mfano, wakinamama kati ya umri wa miaka 15 na 19 wanao uwezekano wa kufariki mara mibli ikilinganishwa na wakinamama ambao wenye umri kati ya miaka 20 na 24.

7. Matokeo ya ndoa za utotoni husababisha upotevu wa fursa kwa mtu binafsi, jamii na nchi.

HATARI ZAKE

KWA FAMILIA NA JAMII

IDADI YA WATU INAKUWA JUU SANA

UPOTEVU WA KIPATO KWA 50% YA WANANCHI (WANAWAKE) - UPOTEVU WA FURSA

HAKUNA MAENDELEO KATIKA JAMII NA NCHI

HAKUNA MAENDELEO KATIKA JAMII NA NCHI

UMASKINI HUJIENDELEZA

WASICHANA

UMASKINI

UKOSEFU WA ELIMU

UKOSEFU WA UJUZI

UKOSEFU WA AJIRA

AFYA MBAYA

Ndoa za utotoni ni suala ambalo haliwaathiri wasichana tu - nchi nzima inapoteza fursa za kujiendeleza!

INATOKEA WAPI?



Kote Tanzania, msichana 1 kati ya 3 wanaolewa kabla hawajafika umri wa miaka 18.

Ndoa za utotoni zinatokea sana katika mikoa ya **SHINYANGA**, **TABORA**, **DODOMA** na **MARA**. Kwa mfano, katika mikoa hayo **ZAIDI YA 50% YA WASICHANA WALIOLEWA** kabla hawajafikia umri wa miaka 18.

Katika mkoa wa **IRINGA**, msichana 1 kati ya 10 ameshaolewa kabla hajafika umri wa miaka 18 na msichana mmoja kati ya watano wa **DAR ES SALAAM** ameshaolewa; haya ni maeneo wapi ndoa za utotoni haitokei sana.

Ndoa za utotoni hutokea zaidi kwenye **MAENEO YA VIJIJINI** wapi umaskini umeenea zaidi, elimu ya sekondari haipatikani kwa urahisi na hakuna elimu nyingi kuhusu afya ya uzazi (k.v. uzazi wa mpango) ukilinganisha na maeneo ya mijini.



ASILIMIA ZA JUU NA CHINI KWA MKOA

UENEAJI WA KIWANGO CHA CHINI KABISA

UENEAJI WA KIWANGO CHAJUU ZAIDI

KWA NINI INATOKEA?

Sheria ya Ndoa ni tofauti kwa wavulana na wasichana: **INAWARUHUSU WASICHANA WAOLEWE WAKIWA NA UMRI WA MIAKA 14** wakati wavulana wanahitaji wawe na miaka 18. Hivi hii ni sawa?

Wasichana wengi wanafundishwa kuanzia umri mdogo sana kuolewa na kuzaa. **ELIMU HAIPEWI KIPAUMBELE** kama vinginevyo. Hii ni tofauti na wavulana wapi wanatakiwa kuilisha familia zao.

KUTOKUWA NA FURSA ZA KUPATA ELIMU na kutokuwa na uwezo wa kupata elimu inasababisha wazazi waachie wasichana wao waolewe.

UMASKINI! Wazazi wanaachia wasichana wao waolewe ili waweze kupokea mahari. Inamaanisha pia kwamba watakua na upungufu wa mtu mmoja wa kumlisha.

TABIA ZA KIUTAMADUNI nyingine kama ibada za kufundwa, ngoma za kienyeji na ukeketaji zinawataharisha wasichana wawe tayari kuolewa pale mwanzo wanapoanza kubalehe. Na pale msichana anapopitia vitu hivi, wanajulikana kuwa tayari kuolewa.

UPUNGUFU WA ELIMU kuhusu afya ya uzazi kati ya wasichana na wavulana inasababisha **WASICHA KUPATA MIMBA**. Matokeo yake ni kwamba wanalazimishwa kuoana na baba wa mtoto hata kama hawataki.

Wazazi wengi wanaogopa kwamba wasichana watavyopata mimba, wataleta "**AIBU**" kwa familia zao, hii ndio maada wanakubali wasichana wao waolewe ili **WALINDE SIFA ZA FAMILIA**.

INAWEZA KUMTOKEA MTU AMBAYE NAMJUA?

Inaweza kumtokea mtu ambaye namjua?



Inatokea kwa wasichana zaidi kuliko wavulana.

Wasichana ambao wanatoka familia maskini wanayo uwezekano mkubwa zaidi kwa mara mbili ukilinganisha na wasichana ambao wanatoka familia tajiri zaidi.

Wasichana wa vijijini wapo katika hali ya hatari zaidi kuliko wasichana wa mijijini.

Ukosefu wa fursa za kwenda shuleni huongeza hatari ya ndoa za utotoni kutokea.

Wasichana wanayo ruhusa ya kuolewa kuanzia umri wa miaka 15 wakati wavulana wanatakiwa kusubiri mpaka wakiwa na umri wa miaka 18. Huu ni ubaguzi na wasichana wenye umri chini ya miaka 18 hawapewi ulinzi kamili wa sheria.

Ujauzito kati ya vijana huongeza ndoa za utotoni kutokea pamoja na matatizo ya afya.

Wasichana wa kabila ambazo wanafanya ibada za kufundwa, ngoma za kienyeji na ukeketaji wapo kwenye hali ya hatari kwasababu shughuli hizi uwa hupendekeza ndoa za utotoni.

Wasichana ambao wanatoka familia za wafugaji wapo katika hali ya hatari zaidi kwasababu mifugo inathaminiwa kuliko wasichana.

NINI KINAWEZA KUMTOKEA?

Matokeo ya ndoa za utotoni.



SHERIA INASEMAJE?

Tanzania imesaini mikataba ya kitaifa na kimataifa ambazo hazikubali ndoa za utotoni. Mtoto ni mtu yoyote aliyekuwa na umri chini ya miaka 18!

Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kutokomeza aina ZOTE za Ubaguzi dhidi ya Wanawake inasema: **"KILA NCHI INAPASWA KUWEKA UMRI WA CHINI WA KUOLEWA NA KUFANYA NDOA ZA UTOTONI ZIWE KINYUME CHA SHERIA."**

Mkataba juu ya Ridhaa ya Ndoa inasema: "Umri wa Chini wa Ndoa na Usajili wa Ndoa hulazimu mataifa kuanzisha umri wa chini wa ndoa na **KUSAJILI NDOA ZOTE."**

Azimio la Haki za Binadamu linasema: **"MTU LAZIMA AWE NA UMRI KAMILI WAKATI ANAINGIA KATIKA NDOA NA NI LAZIMA AWE AMEINGIA KWA UHURU NA KWA RIDHAA YAKE KAMILI."**

Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Watoto inazuia ndoa za utotoni na inasema kwamba **KILA MTOTO AWE NA HAKI YA KUPATA ELIMU.**

SHERIA YA MTOTO YA 2009 TANZANIA inazo sheria zinazowalinda watoto kutoka ndoa za utotoni ikiwa ni pamoja na Sheria ya Masharti Maalum Katika Makosa ya Kimapenzi ambayo inafafanua **MTOTO KAMA MTU MWENYE UMRI CHINI YA MIAKA 18.**

TUNA PAMBANA VIPI NA NDOA ZA UTOTONI?

ONGEENI! NDOA ZA UTOTONI ZINAZO MATOKEO MABAYA KWA WATOTO NA JAMII ZAO.

WAELEMISHE NA KUWAWEZESHA WASICHANA WAWEZE KUKATAA NDOA ZA UTOTONI.

WASAIDIENI WASICHANA WAPATE ELIMU! WATAWEZA KUSAIDIA KWENYE KULISHA FAMILIA ZAO.

ZITANGAZENI HAKI ZA WASICHANA KUPATA ELIMU NA KUMCHAGUA MWENZI.

WAELEMISHE WANAJAMII, PAMOJA NA WASICHANA NA WAVULANA, KUHUSU AFYA YA UZAZI NA UZAZI WA MPANGO.

WAPENI WASICHANA SEHEMU SALAMA YA KWENDA WAKIWA WANATOROKA NDOA ZA UTOTONI.

TUBORESHE SHERIA ZA NDOA ZIWE ZINAKATAA NDOA ZOTE ZA UTOTONI KWA WAVULANA, WASICHANA, NA WOTE WALIYO CHINI YA MIAKA 18.

WASHTAKI WATU AMBAO WANAFANYA NDOA ZA UTOTONI.

WWW.MCGDC.GO.TZ/INDEX.PHP/HIGHLIGHTS/MORE/CHILD_MARRIAGE_SURVEY_2017